# USHIRIKA

. . . amini,
Mambo yote yanawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

2 Tunaweza tu kuinamisha vichwa vyetu tena, kwa muda kidogo tu wa maombi.

3 Bwana mwenye rehema, kwa kweli tunashukuru kwa ajili ya kusanyiko hili asubuhi ya leo, na yale macho yetu yameona, na masikio yetu yamesikia. Bariki kila kitu tufanyacho kwa utukufu Wako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

4 Mwaweza kuketi. Pongezi hiyo nzuri kutoka kwa Ndugu Carlson, ndugu hawa wengine, Ndugu David duPlessis, na Ndugu Arganbright, watu mbalimbali, Ndugu Cash, kwa namna fulani ningeweza tu kuzungumza juu ya jambo hilo, kutoa hotuba ya siku nzima juu yake. Nizungumze na Ndugu Arganbright tena, kule kufufuliwa kwa maskini mtoto yule aliyekufa, alikuwa amekufa tangu saa tatu asubuhi hiyo, na hiyo ilikuwa saa nne na nusu usiku huo, taarifa ya daktari. Na mambo ambayo Bwana amefanya, Yeye . . .

5 Mimi na Ndugu Arganbright tukizungumza kuhusu wakati wale wachawi walipokuja, wakaketi pande zote mbili, wakajaribu kuniroga, na kuleta hiyo dhoruba. Hema nusura lipeperushwe, hicho kitu kikubwa, ndipo ikakomeshwa. Nikanena na Mungu, mawingu yakarudi pande zote mbili, huku wakomunisti wakikimbilia madhabahuni na kutoa mioyo yao kwa Kristo.

6 Yale mambo makuu yaliyotukia mkutanoni, Ndugu Cash, jinsi alivyonena pale jinsi Mungu alivyokuwa amembariki.

7 Sasa, hivyo ndivyo . . . Wakati niliposikia Pentekoste kwa mara ya kwanza, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Hilo kidogo ni ninii tu . . . Hao jamaa wangehubiri mpaka wanaishiwa na pumzi, na ungeweza—ungeweza kuwasikia wakivuta pumzi umbali wa nusu maili, karibu hivyo.

8 Nilikuwa nimezoea kubeba Biblia kwapani mwangu, mwajua. Nilikuwa, nilipotawazwa katika Kanisa la Baptisti ya Kimishenari, nikasema, "Mimi ni mhubiri." Mnaona?

Nilipomsikia mmoja wao akihubiri, walisema, "Je, wewe ni mhubiri?"

Nikasema, "Sidhani." Yote ambayo mimi . . . Wangeweza kuhubiri . . .

9 Ninakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo tu, baba yangu alikuwa mpanda farasi, naye alikuwa akiendesha farasi sana,

akaumia. Ndipo nikawazia walinihitaji niende Magharibi kuwafunza farasi, mwajua, kwa sababu nilikuwa nikipanda farasi wetu mzee wa kulima, wajua, Ndugu Tom, baada ya kuwa kidogo amechoka alasiri. Nami ningempanda na kutoa kofia yangu, na kuweka magugu ya miiba chini ya tandiko na kulivuta chini, basi nilifikiri nilikuwa mpanda farasi.

10 Nilipofika huko Magharibi na kuona hao farasi kweli wangeweza kurusha mateke, mtu fulani akaja pale, na kusema, “Je, wewe ni mpanda farasi?”

Nikasema, “Sidhani.”

11 Hakika hufanya ninii, kujisikia tofauti unaposikia kitu kama hicho.

12 Ninataka uone, Ndugu Cash, kilicholeta mafanikio yake, nilichosikia ndicho, alimtanguliza Mungu katika kila kitu alichofanya. Unaona?

13 Ndugu David, naye akinena pale jinsi ambavyo Mwili wote ulivyoungana na kushikamanishwa pamoja, hilo ni zuri sana, hiyo ni kweli kabisa, Ndugu David. Tunapoweza . . . Kila mmoja wetu ana huduma tofauti, kila mmoja hufanya kazi tofauti; kila mmoja wenu ana huduma, huduma tofauti. Wote wanaoingia katika Kristo wana huduma. Hiyo ni kweli. Si mhubiri tu, bali una huduma kwa jambo fulani, wewe, jambo unaloweza kufanya. Na, ninatumaini hili halisikiki la kukufuru, lakini kwa kawaida Mungu hana budi kukusukuma uingie katika huduma yako sahihi.

14 Baadhi ya ndugu wa Kimethodisti, hivi majuzi, ndio kwanza wampokee Roho Mtakatifu, wao ni wakulima huko Indiana, na loo, walikuwa tu wakiwaka moto. Naye akasema, “Nimekuwa nikisoma vitabu fulani,” kasema, “Ndugu Branham, je, sote tuje pamoja sasa na kuitafuta huduma yetu?”

15 Nikasema, “La, mtajiangamiza kwa kufanya hivyo.” Nikasema, “Msifanye hivyo.” Nikasema, “Mtu ambaye daima anamtafuta Mungu kufanya jambo fulani, kuchunguza na mambo *kadha-wa-kadha*, kwa kawaida hana faida sana. Ni mtu yule asiyetaka kulifanya, huyo ndiye Mungu anaweza kumtumia. Mnaona, angalieni—mwangalieni Musa, na Paulo, na watu mbalimbali wakiitoroka, wakijaribu kuikwepa.

16 Hebu mchukue jamaa ambaye daima ni, “Bwana, nitafanya *hili* kama utafanya *hili*,” na mambo kama hayo, Mungu anajua angekuwa na kiburi, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo Yeye huchukua tu mtu ambaye hataki kulifanya, na kusema, “Labda ninaweza kumtumia kwa muda kidogo, mpaka atakapokuwa mmoja.”

17 Kwa hiyo hiyo ni karibu hivyo, ni, unajaribu kulikwepa wakati wote. Huduma kuu sikuzote zimekuwa ni mtu fulani akijaribu kuikwepa, mnaona, si mtu ambaye daima . . . Kwa sababu, acha Mungu awafanyie jambo fulani, ndipo basi

wote wanajivuna, wakubwa, "jinsi walivyo wakuu," na kila kitu. Lakini mtu ambaye hataki kulifanya, ninii tu, yeye alilazimishwa tu kulifanya, halafu anataka kuliondokea upesi awezavyo, atoweke. Na hivyo kwa kawaida ndivyo Mungu anavyofanya kazi. Sasa hili, nisingetaka kusema hilo huko nje kwenye uamsho mahali fulani, lakini hapa kwenye kiamshakinywa . . .

18 Na jinsi ninavyomthamini Ndugu Carlson, Wafanyabiashara wote Wakristo, Ndugu Boze, na huyu Ndugu Sullivan, nadhani ameondoka tena, lakini hakika yeye ni mtu mmoja mzuri mliye naye hapa, huyo Ndugu Sullivan. Yeye ni muungwana sana, na—nampenda kweli. Nami nafikiri, hata hivyo, tunahitaji watu zaidi kama Ndugu Sullivan, yeye ni mtu mzuri sana, mwema sana. Nasi sote tunampenda, naye ni kama mshamba tu kabisa, nami napenda hilo, maana mimi ni mshamba, pia, mwajua, "Ndege wafananao." Kwa hiyo yeye . . . kile tu . . .

19 Ninaamini Ndugu Sullivan ni mtu, ni—ni wa kawaida tu, na kama tusemavyo, huko chini Kentucky, "kabwlea" tu, mwajua. Ni wangapi wanaojua *kabwela* ni nini? Waangalieni Wakentaki. Vema, karibu nililelewa juu yake, chai ya makabwela, sukumawiki. Ah, Ndugu Evans, aliangalia hapa, na kucheka wakati niliposema, sukumawiki, wanazo huko Georgia, pia. Zinachipuka mapema kidogo kule, kuliko zinavyofanya huku juu.

20 Lakini ile mikutano, tukirudi kwenye mikutano yetu, mikutano yetu imekuwa mizuri sana juma hili, Bwana ametubariki sana. Nasi tunaamini tunawaalika kwa ajili ya Ndugu duPlessis, na mimi, na Ndugu Sullivan, na wengi wa wahudumu hapa, tutaendelea usiku wa leo na kesho alasiri, kuwaombea wagonjwa, Mungu akitusaidia.

21 Sasa, ninataka kusoma fungu dogo tu la Maandiko linalopatikana hapa katika Waebrania mlango wa 9, kuanzia kifungu cha 6. Na hebu tusome sasa, kwa ninii tu . . . Hebu tuanzie, naam, kwenye kifungu cha 6:

> *Basi vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani waliingia katika hema hiyo ya kwanza daima,* kutimiza *ibada ya Mungu.*
>
> *Lakini katika hema hiyo ya pili kuhani mkuu huingia peke yake, mara moja kila mwaka, wala si pasipo damu, aliyoitoa kwa ajili ya nafsi yake, na kwa dhambi za kutokujua za hao watu:*
>
> *Roho Mtakatifu akionyesha neno hili, ya kwamba njia ya kupaingia patakatifu pa patakatifu . . .* haikufanywa—*ilikuwa . . . haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali imesimama:*
>
> *Ambayo ilikuwa ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa, wakati huo ambapo sadaka na dhabihu zilitolewa,*

*zisizoweza kumkamilisha mtu aabuduye kwa jinsi ya dhamira;*

*Kwa kuwa ni sheria za vyakula tu...vinywaji,... kutawadha kwingine kwingine,...taratibu kwa ajili ya mwili, zilizoamriwa hata wakati wa matengenezo mapya.*

*Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyizwa kwa mikono, maana yake, isiyo ya jengo hili;*

*Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele kwa ajili yetu.*

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

22 Sasa, kumekuwa na mengi sana ambayo yamesemwa hivi kwamba kwa namna fulani najisikia kama ningekuwa nikiwawekea muda mwingi wa ziada kushughulikia jambo hilo jinsi ninavyoamini hilo lingeweza kuwa kama ingalikuwa huko nje mkutanoni. Lakini kwa matamshi machache tu au maoni kama muktadha kwa ajili ya hili, ningetaka kuchukua somo asubuhi ya leo la *Ushirika*. Niliona kila mmoja akinena juu ya ushirika.

23 Sasa, kwa nini mwanadamu na kwa nini tunakusanyika, kama vile tumefanya mara nyingi, kushiriki pamoja? Ni kitu gani kinachofanya viamshakinywa hivi viwe vya kuvutia sana, kama vile Ndugu duPlessis alivyosema dakika chache zilizopita? Ni, nitakubaliana naye, ni moja ya nya—nyakati za kuvutia sana za maisha yangu, ni kuungana na kundi hili la watu waliochanganyikana wa madhehebu mbalimbali, na kuja pamoja, na kula na kufanya ushirika, ushirika kwanza.

24 Nasi tunaona kula kunadokezwa katika ushirika. Kwa nini tunakula kiamshakinywa? Mbona, tunakutana tu na kuzungumza, lakini kuna kitu kuhusu kula kinacholeta ushirika.

25 Na sasa, mlimwona Yesu katika ku—kumalizia kwa safari Yake ya maisha? Alitaka muda kidogo wa ushirika pamoja na wale wanafunzi, kwa hiyo akawaita kando, na kuandaa meza, na kumega mkate, na—na—na kuubariki, nao wakala. Nacho chakula cha mwisho kilikuwa ni ushirika pamoja na wanafunzi Wake, kabla tu hajavuka kuingia katika ile Nchi nyingine kuwa Kuhani wetu Mkuu.

26 Nami nafikiri, leo hii, ninapoangalia huku na huku na kuwaona matajiri, watu maskini wote wakishiriki pamoja, kuna

jambo kulihusu tulilo nalo kwenye misingi ya maslahi ya pamoja, hilo ni ushirika wa Kikristo.

27 Na kila mtu, labda mtu huyo ni ninii, mtu fulani alinena, kama yule ndugu aliyekuwa akisema ya kwamba Bwana alikuwa amembariki kwa kiasi *kikubwa* cha pesa, na hao watu wengine, labda unafikiri huna kiasi hicho cha pesa, wala hutaki kutoa ushuhuda wako, bali Mungu amekupa kitu fulani, ni kama vile Ndugu duPlessis alivyosema, kwamba Yeye hajampa mtu *huyu*, ni tofauti kabisa.

28 Hamjui jinsi nilivyojisikia hivi majuzi nilipokuwa huko Tulsa. Nilipitia kwenye mkutano wa Ndugu Osborn, ama, mahali pake pa biashara. Na Tommy Osborn ni Ndugu mzuri sana Mkristo! Basi akanionyesha ramani yake ya kila mahali alipokuwa na wamishenari, mamia yao kote ulimwenguni, akanikumbatia kwa mikono yake, akaanza kulia, akasema, "Ndugu Branham, wewe ndiwe, kwa huduma yako, uliyenituma kwenda kufanya jambo hili." Akanipa kijisanamu cha sanamu ya mtu na mwenyeji aliye na bloku kinywani mwake. Kasema, "Hebu wazia tu juu ya huduma yetu, ni wangapi wao tumewakomboa kutoka kwenye hiyo."

29 Nikaangalia kazi kuu ya Tommy pale, na, loo, jinsi ilivyokuwa nzuri sana, na mahali pazuri sana! Na watu wote, jinsi walivyokuwa ni kundi lililotakaswa, na jinsi wanavyompenda Bwana, na kuja pamoja katika kanisa dogo kuabudu. Nami nikazungumza nao kisha nikaanza kulia.

30 Ndipo nikashuka kwenda kwa Ndugu Oral Roberts, mtu mwingine mashuhuri, na mtumishi wa Mungu, mnyenyekevu. Alijeruhiwa nilipokuwa kule, huku nikienda tu jukwaani, akaagizia nije upesi nikamwombee. Goti lake, sijui kama alilivunja, ama kilichokuwa kimetukia. Basi nilipokuwa nikiomba, mishipa ya damu ilikuja pamoja na kufanya alama ya V kubwa juu ya goti lake. Ndipo nikaweka mkono wangu juu yake na utukufu wa Mungu ukashuka chumbani mwake mle, ndipo akasimama, akaja mlangoni pamoja nami. Na mtu mzuri sana.

31 Ndipo nikaangalia kwenye jengo lake kubwa mno. Kama umewahi kuwa na majaliwa ya kuliona, bila shaka ni u—u—ukumbusho wa imani ya mtu mmoja, kile anachoweza kufanya wakati anapoanza kulitekeleza. Loo, kamwe sijaninii… Nimekuwa Hollywood. Nimekuwa katika sehemu zote mbalimbali, sijawahi kuona kitu kama ninii, jengo lile huko Tulsa, la Ndugu Roberts, jinsi lilivyotengenezwa katika umbo la utatu.

32 Na kila kitu mle ndani kina ninii—ninii…marumaru ya kutoka nje ya nchi, na ni mahali pazuri jinsi gani! Nami… Hakikisheni mmekiona hicho kioo. Nilipotoka kwenda kuona hilo, mikono hiyo ikifikia kikombe cha baraka, nilikuwa tu

nikilia kwa furaha kujua kwamba . . . Hata dari, iliyotengenezwa kwa nyaya ndogo za aluminiamu zilizofumwa pamoja, kamwe sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu, na kuwazia ya kwamba maskini mvulana mmoja, aliyezaliwa shimoni huko Oklahoma, alitimiza hilo, kwa imani.

33 Nilisimama nje, ndipo nikaanza kuwazia hilo, hakuna mtu aliyekuwa pamoja nami, Ndugu Fischer alikuwa amenipitisha, nilikuwa nikiangalia kote, nikawaza, "Ee Mungu, kuwazia, huduma ya Ndugu Oral ilitokana na yangu, huduma ya Ndugu Osborn ilianza kutoka kwa yangu, nami ningeona aibu wakiiona ofisi yangu: taipureta moja ndogo iliyowekwa mwishoni mwa trela. Hiyo ni kweli, taipureta moja ndogo."

34 Ndipo nikawazia, "Vema, Yesu hata hakuwa na ofisi, kamwe hakuwa na ofisi kabisa, kamwe hakuwa nayo. Hakuna mahali katika Biblia paliposema Yesu alikuwa na ofisi."

35 Ndipo nikasimama pale na kulia kwa furaha kuona jinsi Mungu alivyokuwa amembariki ndugu yangu, ndipo nikaanza kuwazia, kitu fulani kikaniambia, "Lakini vipi kukuhusu wewe, unaona?"

36 Nikasema, "Vema, hapana shaka mimi ni mnafiki tu. Hapana shaka kwamba Mungu hata asingeweza kunitumainia. Mimi—mimi—mimi . . . Labda hiyo ndiyo sababu."

37 Ndipo nilipokuwa nimesimama pale, huku machozi yakitiririka mashavuni mwangu, nilitazama jengo hilo kubwa mno, Kitu fulani kikanena nami, na kusema, "Lakini mimi ndiye Urithi wako."

Nikasema, "Vema, Bwana."

38 "Ni—nitakuwa Urithi wako." Mnaona? Kwa sababu sina uwezo wa elimu kushughulikia mambo makuu namna hiyo, ambayo Bwana amewapa ndugu zangu walio na uwezo. Lakini mradi tu nitaendelea hivi! Mnaona?

39 Sasa, ninajua jinsi mfanyabiashara fulani angejisikia kumsikia mtu huyo, jinsi Mungu anavyobariki, lakini kumbukeni, "Mungu ndiye Urithi wako, pia, ndugu. Mungu ndiye Urithi wako." Tunapokusanyika pamoja, ushirika wetu ni sawa, unaona, tunafanya ushirika mmoja na mwenzake.

40 Na sasa, ilisema hapa, ya kwamba—ya kwamba Kristo aliingia mara moja tu katika Ma—Maskani. Sasa, tunaona ya kwamba ushirika msingi wake ni mapatano, haina budi kuwa hivyo, maana ushirika ni jambo tunalopenda kufanya, kuja pamoja.

41 Ni kama tu kijana mwanamume na kijana mwanamke wakikutana, nao ni, wanapendana, na kamwe hawawezi kabisa kukaa bila kuonana. Tunajua, ndugu, jinsi tulivyojisikia, na kina dada, jinsi ulivyojisikia ulipokutana na mume wako, na—na kuna ushirika. Kila usiku, huwezi tu kungojea mpaka

wakati wa miadi yako, nawe unataka kumpeleka mahali fulani mkale chakula, nawe unaweza kuketi na kuzungumza, na kumwangalia, na ni—ni ushirika. Unaona?

42 Na sasa, kabla huo haujaweza kuwa ushirika, hauna budi kutegemea mapatano, mnaona, juu ya mapatano. Na hiyo ni kweli tu iwezavyo kuwa. Naye Mungu, kabla hatujaweza kufanya ushirika Naye, kwanza, yote yanayotufanya tutake ushirika ni, kwa sababu ni *kitu fulani* ndani yetu kinachouhitaji.

43 Sasa, ushirika katika mambo ya mapenzi, kama kijana mwanamume na kijana mwanamke, huo ni ushirika, na kile tungekiita, neno la Kiyunani la *fileo*, huo ni upendo tu wa duniani. Lakini ushirika katika Injili, namna hii, ni *Agapao*, Kiyunani, "upendo wa juu, wa Kiungu," kama nilivyozungumza usiku uliopita juu ya ono langu.

44 Unapokuwa mle ndani, si mwanamume wala mwanamke, wao ni—wao ni, sisi sote ni mmoja tu katika Kristo. Nasi tunapaswa kupata uzoefu wa ushirika wa namna hiyo hapa duniani, wakati tukiwa na, lazima tuwe na heshima mmoja kwa mwenzake, na upendo sisi kwa sisi, wenye mawazo ya hali ya juu sana kwa ajili ya dada zetu na ndugu zetu, na kamwe kusiweko na jambo lolote baya, lazima tusiliache liingie akilini mwetu, tulifutilie tu mbali, kwa sababu sisi ni raia wa Ufalme wa Mungu, sisi ni watu walioitwa watoke na waliotengwa. Hiyo ndiyo sababu tungeweza kuingia na heshima ya Kikristo, pamoja na wanaume halisi na wanawake halisi wenye mawazo ya hali ya juu sana na—na walio bora sana mmoja kwa mwingine. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa nayo.

45 Sasa, Mungu alitaka ushirika. Na kama sisi, haijalishi, kama mwanaume leo hii ni mwana wa Mungu aliyeanguka, kuna baadhi ya sehemu za Mungu ambazo zingali pamoja na mtu huyo katika hali yake ya kuanguka. Hebu mchukue mtu leo hii anayeweza kupasua atomi, ama molekuli, ama chochote unachotaka kuiita, na anaweza kuendesha ndege ya jeti kuuzunguka ulimwengu katika saa chache, nawe unaweza kuona kwamba ndivyo alivyo, kitu fulani ndani yake ni kiumbe kilichoanguka. Sasa, hawezi kuumba chochote, lakini anaweza kupotosha kile kilichoumbwa kikawa kitu cha kujiboresha.

46 Basi hiyo inaonyesha ya kwamba mwanadamu kamwe hakutoka kwenye uhai wa wanyama, maana mnyama daima hujenga makao yale yale ya kuishi. Lakini mwanadamu hujitengenezea nyumba bora, njia bora ya kuishi, nguo bora, na usafirishaji bora. Sasa hayo yote yanaonyesha ya kwamba kitu fulani nyuma . . . hata katika hali yake ya kuanguka, yeye angali ni mwana wa Mungu, aliyeanguka.

47 Ndipo basi anapotaka ushirika, na tunapotaka uchumba na mambo kama hayo, hayana budi kuja juu ya msingi wa mapatano. Sasa, Mungu alipomwumba mwanadamu hapo

mwanzo apate kushirikiana naye, basi mtu huyu alikuwa katika ushirika mkamilifu katika bustani ya Edeni, alikuwa katika ushirika mkamilifu na Mungu. Na jinsi ambavyo hapana shaka ilikuwa katika siku ile ambayo Mungu angeshuka wakati wa jua kupunga na kumwita Adamu, yeye na Hawa wangekuja, nao wangemwabudu Mungu, kisha wangefanya ushirika na kushirikiana, mmoja na mwenzake!

48 Hicho ndicho kitu hasa kinachotuleta pamoja namna hii, tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukishirikiana katika Roho Mtakatifu. Hakuna tofauti ndani yetu, sisi sote ni mmoja katika Kristo Yesu, katika upatanifu huo mkamilifu wa ushirika. Hakuna kitu kama hicho nilichowahi kupata duniani, ni kukusanyika pamoja katika ulimwengu wa Roho na kufanya ushirika, kushirikiana na Mungu na sisi kwa sisi. Sasa, hilo ndilo Mungu alilokusudia katika bustani ya Edeni.

49 Ndipo ushirika huo kutoka kwa Mungu na mwanadamu ukavunjwa na dhambi. Sasa, Mungu alifanya msingi na mahali ambapo mwanadamu angeweza kubaki, ama kudumisha, ushirika wake, nao haukuwa ni kupitia kwenye mkutano, ama shirika, ama—ama elimu, ulikuwa juu ya msingi wa damu iliyomwagika. Na hapo ndipo mahali pekee pa ushirika tulipo napo pamoja na Mungu siku hizi, na mahali pekee pa kukutania ni kupitia Damu ya Yesu Kristo. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona?

50 Sasa, tumejaribu kufanyia ushirika madhehebu; unajitenga na kundi lingine unapofanya hivyo. Vema. Tulijaribu kuwaelimisha wafanye ushirika. Nasi tunapata nini? Mbona, tunapata kundi la mabaradhuli wenye elimu. Na hilo—hilo—hilo ni jambo la kuchukiza sana kwa mhubiri kutoa tamshi kama hilo, lakini hilo, hilo ni kweli.

51 Mimi—mimi. . .Jambo fulani lilinifanyikia majuma machache yaliyopita, nami nimeazimia, kwa msaada wa Mungu, kamwe nisiwe kinyume juu ya chochote, tena, kuulipua moyo wangu, kukumbusha, haidhuru itagharimu nini, mnaona, niwe mwaminifu kabisa, na hiyo ni kweli.

52 Nao watu wanajielimisha tu mpaka wataninii, wanajielimisha hata wakatengana, wanapata vinyongo. Hupati kinyongo chochoote kwa Damu ya Yesu Kristo, unapata upendo, hapo ndipo, hiyo ni, unapata upendo, si kinyongo, ati "Mimi ni mkubwa kidogo kuliko mtu mwingine, bora kidogo kuliko mtu mwingine, najua zaidi kidogo kuliko mtu mwingine." Unamkumbatia tu kila mtu, na ni msingi wa upendo kupitia Damu, Damu husafisha.

53 Sasa, ushirika huja kwa upendo; nao upendo unahitaji ushirika. Kama unampenda mke wako, inakubidi tu kukutana naye na kuzungumza naye; kama unampenda rafiki yako, huna budi kukutana naye na kuzungumza naye; na kama unampenda

Mungu, hapana budi pawe na msingi wa ushirika. Huwezi kuwa na ushirika mkamilifu na—na riziki bila mapatano haya.

54 Huwezi kufanya ndoa bila mapatano, huwezi kuwa na mke pasipo namna fulani ya mapatano. Na mapatano hayo yanategemea nadhiri zako. Huwezi kuwa na ushirika na Mungu pasipo kufikia mapatano na Mungu, na kuna jambo la msingi kwa ajili ya ushirika, na hilo ni damu, damu pekee. Imekuwa ni njia ya Mungu tangu mwanzo, na itakuwa hivyo hata mwisho. Mahali pekee pa ushirika ni kupitia damu.

55 Sasa, tunaona katika Agano la Kale, ya kwamba Mungu alikuwa na mahali pamoja pa kukutania, mahali pamoja pa kukutania, mahali pekee Yeye angekutana na watu Wake palikuwa ni mahali pamoja, maskanini, na hapo palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. Mahali pekee Mungu alipokutana na watu Wake, palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika; hapo ndipo mahali pekee anapoweza kukutana nasi siku hizi.

56 Hawezi kukutana nasi kama dhehebu, hawezi kukutana nasi kama kundi la wasomi, Yeye anaweza tu kukutana nasi tunapofanya ushirika, tunapokuja chini ya Damu iliyomwagika ya Mwanawe, Yesu Kristo, hapo ndipo mahali pekee pa kimsingi tunapoweza kukutania.

57 Wakati fulani uliopita, nilikuwa nikiweka wakfu maskani, wakaniomba niyalete tena ma—maneno hayo, ndugu fulani huko Tennessee, ninasahau jina lake lilikuwa ni nani sasa, Church of God, kule chini, nami nikasema, “Mungu ni Kiumbe.”

58 Sasa, Mungu si tu kama ninii yako. . .kama hewa, kama angekuwa hivyo, kamwe haingekubidi kumtafuta Roho Mtakatifu, angekuwa ndani yako, maana Yeye angejaza anga lote na kadhalika. Mungu yuko kila mahali, hakika, kwa kujua yote, akijua mambo yote. Lakini Mungu ana makao, kwa sababu Yeye ni Kiumbe. Kweli kabisa. Na Mungu anaishi kwa ushirika chini ya Damu iliyomwagika ya Mwanawe, na hiyo pekee. Amina. Sio juu ya madhehebu yetu ama ushirika wetu, bali juu ya Damu iliyomwagika tunakutana na Mungu uso kwa uso.

59 Sasa, Ayubu aliamini hilo, Kitabu cha kale kuliko vyote katika Agano. Mungu alikutana na Ayubu juu ya msingi wa ushirika, kupitia sadaka ya kuteketezwa na damu iliyomwagika. Kumbukeni, Ayubu, yeye alisema, “Sasa, labda watoto wangu wametenda dhambi, na kama wametenda dhambi, nitatoa tu sadaka ya kuteketezwa,” kwa sababu hiyo tu ndiyo Mungu aliyohitaji. Mungu alihitaji tu damu iliyomwagika, sadaka ya kuteketezwa. Naye Ayubu akatoa sadaka kwa ajili ya watoto wake.

60 Nasi tunatambua kilichotukia wakati huo ambapo dhoruba ilikuja na kuwaua watoto wake, ikawachukua mifugo wake wote. Nasi tunajua jinsi alivyofadhaika na jinsi alivyokuwa

amechanganyikiwa. Lakini ulikuja wakati ambapo Mungu alirejesha yote kwa Ayubu.

61 Basi alipokuwa huko nje kwenye lundo la majivu, huko, akikwaruza majipu yake, basi mkewe alisema, "Kwa nini usimkufuru Mungu ukafe mauti?"

Akasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu."

62 Ndipo wale watu walipokuja kumbariki, badala yake, walimpa kisogo na kumwita mwenye dhambi wa siri. Ayubu alijua hakuwa ametenda dhambi, kwa sababu alikuwa ametimiza matakwa ya Mungu.

63 Sasa ajali na shida haziwapati watu kwa sababu wao ni wenye dhambi, maana nimewaona wenye dhambi wakifanikiwa na kuendelea. Lakini ni—ni juu ya msingi wa ushirika. Kwa sababu mtu akifanikiwa katika biashara hakumfanyi kuwa Mkristo kwa jumla, maana kuna wenye dhambi wengi wanaofanikiwa. Hiyo ni kweli.

64 Kitu gani? Ushirika wetu hauko juu ya msingi wa jinsi Mungu anavyotufanikisha, bali kwa msingi wa kuja chini ya Damu iliyomwagika, na kushirikiana sisi kwa sisi. Hapo ndipo sehemu halisi ya Ukristo ilipo. Hilo ndilo linaloifanya mikutano hii kuwa halisi sana, hapo watu wanapokuja chini ya misingi hiyo ya Damu iliyomwagika, tuna mambo shirika, tunaketi katika ulimwengu wa Roho.

65 Sasa, Ayubu aliambiwa na mkewe, "Kwa nini usimlaani Mungu, na ufe tu mauti?"

66 Akasema, sasa, hakumwita mwanamke mpumbavu, a— alisema, "Unanena *kama* mwanamke mpumbavu." Hakusema alikuwa mpumbavu, bali alinena hivyo. Kasema, "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; libarikiwe Jina la Bwana," kwa kuwa alijua ya kwamba alikuwa ametimiza matakwa ya Mungu. Alikuwa amemwabudu Mungu chini ya msingi wa damu iliyomwagika na dhabihu ya kuteketezwa, naye akasimama imara juu yake. Haidhuru ni jambo gani lililotukia, angali alijua ya kwamba alikuwa amehesabiwa haki, kwa sababu alikuwa ametimiza matakwa ya Mungu.

67 Haidhuru wanajaribu kukuita mlokole jinsi gani, ama mtakatifu anayejibingirisha, ama chochote wanachotaka kusema, mradi tu unajua umetimiza matakwa ya Mungu nawe uko chini ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo, unasimama umehesabiwa haki katika Uwepo wa Mungu. Si lazima uwe mfuasi wa kundi lolote, inakubidi tu kuwa chini ya mahali hapo kwa ajili ya ushirika.

68 Sasa, Mungu alianza kumrejeshea Ayubu, alirejesha akiba yake, wanyama wake, mifugo, na kila kitu, maradufu. Lakini hivi uliona kuhusu watoto wake? Mungu aliwarejesha watoto wa Ayubu. Hakusema aliwaongeza maradufu, bali alimrejeshea

hao. Unashangaa walikuwa wapi? Je, uliwahi kuwazia jambo hilo katika kusoma Kitabu cha Ayubu? Walikuwa Utukufuni, wakimngojea, kwa sababu alikuwa ametoa dhabihu chini ya damu iliyomwagika, naye alijua mahali walipokuwa wakimngojea, chini ya damu iliyomwagika. Sasa, Yeye kamwe hakusema alimrejeshea kundi lingine la watoto, bali Yeye—Yeye, Mungu, alimrejeshea Ayubu watoto wake, kwa sababu walikuwa wakimngojea chini ya damu iliyomwagika ya dhabihu.

69 Huko nyikani, maskani, kulikuwako na njia iliyowekwa ya ushirika kwa ajili ya mwaminio. Sasa, kitu cha kwanza kilichochukuliwa, walichukua ndama mwekundu, na lazima awe bila doa juu yake. Naye ndama huyu mwekundu alikuwa ni mfano wa Damu ya Yesu, nyekundu. Nyekundu hunena neno baya wakati mwingine, la taa nyekundu, na kadhalika ya hayo, maonyo; lakini damu pia hunena, nyekundu ni rangi ya upatanisho, pia.

70 Uliwahi kuona? Hata katika maisha ya kisayansi, ukichukua nyekundu na kuiangalia kupitia nyekundu kwenye nyekundu, ni nyeupe. Umewahi kujaribu hilo? Angalia nyekundu kupitia nyekundu, ni nyeupe. Ndipo basi wakati Mungu anapomwangalia mwabuduo kupitia Damu ya Mwanawe, haijalishi dhambi zake zinaweza kuwa nyekundu jinsi gani, yeye ni mweupe kama theluji, na tayari kwa ushirika. Nyekundu kupitia nyekundu hugeuka nyeupe.

71 Sasa angalieni, ndama huyu mwekundu hana budi kuchinjiwa nje ya kambi, mfano mkamilifu wa Kristo. Hana budi kuchomwa moto, huyo, awe majivu, kwato, pembe, na vyote pamoja, lazima vichomwe moto kufanya maji ya farakano.

72 Sasa, damu yake ilitiwa katika sinia na kupelekwa na kuhani kwenye mlango wa maskani, na kulikuwa na milia saba iliyowekwa juu ya mlango wa maskani kwa damu ya huyu ndama, ambayo ilimwakilisha Kristo. Sasa, sasa angalieni, loo, ni pazuri hapa, na damu hiyo iliyowekwa mlangoni iliwekwa hapo pamoja na mwerezi, na hisopo, na sufu nyekundu.

73 Sufu nyekundu ilikuwa ni sufu iliyotiwa rangi, na hisopo ilikuwa ni magugu ya kawaida, maua juu yake, na mwerezi ni mti ulio mwekundu na ni mweupe ndani yake. Loo, jamani, nikiingia kwenye mifano hiyo, basi hatutaenda nyumbani adhuhuri, hiyo ni kweli, kwenye mifano hiyo. Ni nzuri jinsi gani!

74 Ninawatakeni mkumbuke jambo moja hapa, hasa, hilo ni, juu ya hisopo. Hisopo ilikuwa ni kupaka . . . Damu ilipakwa kwa hisopo, na hisopo ni ya kawaida kama magugu. Nayo Damu inapakwa kwa imani, kitu cha kawaida, unanyosha mkono na kuiokota popote, unaona, hivyo ndivyo Damu inavyopakwa. Haikubidi kwenda mahali fulani kuipata, unachukua tu magugu, mambo ya kawaida, imani yangu rahisi katika Kristo na kuamini. Nayo Damu inapakwa kwenye mlango wa moyo

wako kwa imani, imani rahisi, mwamini tu Yeye. Sio chochote kinachokubidi uwe tofauti kwa vyovyote, ni imani tu uliyo nayo sasa.

75 Kama kuna watu wagonjwa hapa, ninawapa changamoto mchukue imani hiyo rahisi mliyo nayo na kuitumia, kwa imani, Damu ya Yesu Kristo kwa ajili ya ugonjwa wako uone kinachotukia. Mtu yeyote hapa anayejisikia ya kwamba una karama ndani yako, jambo ambalo—ambalo hujali kulifanya, bali ni jambo tu ambalo Mungu anakusukuma kufanya, paka Damu kwa imani rahisi kwenye hilo, uangalie kitakachotukia. Lijaribu tu mara moja uone. Jitose tu ndani yake, nawe utaona kitakachotukia.

76 Sasa, basi majivu haya ya ndama huyu, jinsi tungeweza kukaa juu ya hilo! Ni somo zuri jinsi gani wakati mwingine katika mkutano wa kambi, ama kitu fulani, kuchukua kila moja ya alama hizo, na kuishusha hisopo hiyo, kuleta mti huo mwekundu wa mwerezi, ambao ulikuwa ni msalaba, na damu, na kadhalika, katika mwerezi huu uliochanganywa nao. Sasa, tungeweza tu kuchukua usiku mmoja juu ya kila moja ya mifano hiyo na kuileta huku.

77 Lakini upesi, angalieni sasa, wamechukua majivu ya ndama na kuyaweka nyuani kwa matumizi ya maji ya farakano, kumwosha asiyeamini katika maji ya farakano kwa ajili ya utakaso, kwa kuwa sasa tunaoshwa kwa maji ya Neno la Mungu, hutuosha.

78 Halafu basi, mwangalieni mwaminio akiingia sasa: Jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kuingia nyuani, na kusikia, na kupokea, jambo la kwanza lililotukia ni kwamba alilichukua Neno kwanza. Alihubiriwa Neno, kama linavyohubiriwa mwenye dhambi, Nalo linatumiwa. Hayo ndiyo Maji ya farakano, kwa kuwa tunaoshwa kwa maji ya Neno. Unaona?

79 Sasa, kile tunachojaribu kufanya, sasa, sikilizeni kwa makini, tunakaribia mahali halisi pa ushirika, kile ushirika halisi wa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu unachomaansha. Loo, kama unaweza kupata wazo hilo, ndugu, umemalizana na kila kitu cha ulimwengu papo hapo, kama unaweza tu kulishika.

80 Sasa, mwaminio huja kwanza na kulisikia Neno, "Imani chanzo chake ni kusikia." Chukua hisopo yako. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Maji ya farakano." Unaona? Huyu asiyeamini akiingia nyuani, jambo la kwanza, kama mtu huyo alikuwa akianguka, jambo la kwanza alilofanya, aliingia nyuani na kunyunyiziwa majivu ya ndama huyu, yaliyoitwa Maji ya farakano, ikionyesha ya kwamba kitu fulani kilikufa, ya kwamba majivu ya ndama huyu yalikufa kwa ajili ya dhambi zake.

81 Hicho ndicho kinacholetwa na kuhubiriwa kwa Injili, Maji ya farakano: Unaanza kugundua kwamba ulikuwa mwenye dhambi, Mtu fulani alikufa kwa ajili yako, Mungu alikupa Neno Lake, akaahidi Damu, Mwana, ndipo unaipokea kwa imani, kwa kupaka hisopo. Unaona, kwa imani unanyosha mkono na kupokea Maji ya farakano, Neno.

82 Sasa, jambo lingine unalofanya, unaanza. . .Hauko katika ushirika, bado; hapo ndipo, ndugu zangu Wabaptisti, hakika sikubaliani na nyinyi. Naam, bwana. Wengi wao wanasema, "Vema, unampokea Roho Mtakatifu unapoamini."

83 Ndipo mtu fulani akaniuliza swali, hapa si muda mrefu uliopita, akaliweka jukwaani, "Ndugu Branham, uliwahi kusoma ile ya asili? Ile ya Kiyunani inasema ya kwamba unampokea Roho Mtakatifu unapoamini."

84 Laiti ungaliniletea hiyo *Diaglott*, laiti ungaliniletea kamusi hiyo ya Kiyunani inayosema hivyo, haisemi hivyo, inasema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Sio, "mlipoamini." Lakini "*tangu* ninyi. . ." Nina ile *Emphatic Diaglott* ya tafsiri asili kutoka kwenye. . .kutoka kwenye—kwenye, kutoka kwenye Mji wa Vatikani, ya Kiyunani asili, halafu nina ya Kiaramu, na zingine nyingi zinazothibitisha kwamba alisema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Walikuwa ni waaminio, naye Paulo akasema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?"

85 Sasa, hawakuwa wameingia katika ushirika mkamilifu bado. Ndipo Paulo akaweka mikono yake juu yao, wakampokea Roho Mtakatifu, ndipo nguvu za Mungu zikawashukia, nao wakanena kwa lugha na kutabiri, *ndipo* wakajazwa na kuingia katika ushirika mkamilifu pamoja na Kanisa lote. Huo ndio msingi pekee.

86 Angalieni, tunakuja kwenye Maji ya farakano, yaliyopakwa kwa hisopo, lile gugu, imani ya kawaida. Basi anafanya nini? Wanamgeuza basi kuelekea mlango wa maskani.

87 Sasa, kabla. . .mle ndani ndimo Bwana alipo kwenye ninii Yake, mahali patakatifu, ndani. Sasa, hata tunaweza kulichukua kutoka mle ndani, na kwenda hadi Patakatifu pa patakatifu, na kadhalika.

88 Lakini sasa, hebu na tulichukue tu hivi: Wakati anapokuja mlangoni, juu ya mlango kuna milia saba ya damu, kabla hajaingia katika ushirika huu, hana budi kutambua ya kwamba damu hii imemsafisha na dhambi zake, ambao ni utakaso, utengano. Baada ya sisi. . .Neno limewekwa, tumelipokea, sasa tunaingia chini ya damu.

89 "Kuna Watatu washuhudiao Mbinguni: Baba, Neno, na Roho Mtakatifu, hawa Watatu ni Mmoja. Wako watatu washuhudiao duniani," Yohana wa Kwanza 5:7, "maji, Damu, na Roho, si mmoja, bali *hupatana* kwa habari moja."

90 Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu *ni* Mmoja, lakini maji, damu, na Roho *hupatana* kwa habari moja, maana unaweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa; huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu, kwa hiyo wao ni Mmoja. Lakini unapohesabiwa haki kwa imani, bado hujatakaswa, wala huwezi kutakaswa . . . na— na utakapotakaswa basi huna Roho Mtakatifu bado.

91 Sasa, zile elementi zilizotoka katika mwili wa Yesu zilikuwa ni maji, Damu, Roho. Kinachotoka katika mwili Wake wa kawaida ndicho kinachojumuisha kuzaliwa upya. Nini—ni nini, mtoto mchanga anapozaliwa, ni kitu gani cha kwanza kinachotukia? Samahani, dada zangu. Kitu cha kwanza kinachotukia ni kipi? Maji hutoka. Cha pili ni kipi? Damu. Kinachofuata ni kipi? Uhai. Kweli kabisa.

92 Kile kinajumuisha kuzaliwa kwa kawaida ni mfano wa kuzaliwa kiroho. Kitu cha kwanza ni kipi? Maji, ni maji ya farakano, kuhesabiwa haki kwa imani kama yule ndugu alivyosoma Maandiko asubuhi ya leo, Warumi 8, ama, Warumi 5, kuhesabiwa haki kwa imani. Ni kitu gani kinachofuata? Kutakaswa, utakaso. Kuchukua ki—kikombe na kukihesabia haki ni kukiokota, kukitakasa ni kukisafisha, ndipo kiko tayari kwa ajili ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Mnaona? Neno *takasa*, ni neno linalomaanisha, "kimesafishwa na kuwekwa kando kwa ajili ya utumishi," bali hakitumiwi.

93 Hapo ndipo mimi . . . Ninyi ndugu wa Nazarayo na Pilgrim Holiness, mnaofikiri kwamba utakaso ndio kazi yote ya Roho Mtakatifu, sivyo, utakaso hukusafisha, lakini Roho Mtakatifu anakujaza. Bilauri inawekwa kando kwa ajili ya utumishi, bali haitumiwi mpaka itakapowekwa katika matumizi na Roho Mtakatifu na kujazwa na Roho Mtakatifu. Mnaona? Jambo ndilo hilo.

94 Sasa, mwangalieni mtu huyu, kwanza, aliipokea kwa yale Maji ya farakano, "Imani huja kwa kusikia." Pili, mti wa mwerezi, anawekwa kwa matumizi sasa. Unaona, yeye—yeye ana . . . Inakubidi kutambua damu inayomtakasa, yeye bado hajaingia Kanisani, yeye bado hajaingia kwenye ushirika, lakini yuko njiani kuelekea humo. Amelisikia Neno, "Imani chanzo chake ni kusikia," ndipo anaangalia na kutambua hiyo milia saba.

95 Tungalikuwa na wakati wa kuchukua hilo, ile milia saba ilimaanisha zile nyakati saba za kanisa, ama vile vipindi saba vya wakati, ama chochote unachotaka kuziita, kwamba katika kila wakati Mungu huitambua tu damu. Mnaona?

96 Kutoka Mwanzo hadi mwisho wa Ufunuo, damu ndiyo inayosafisha. Mchirizi huo mwekundu umepitia kote katika Biblia kutoka jalada moja hadi jingine. Msingi wa ushirika ni kupitia kwa damu. Ni kweli kabisa. Misingi pekee ya msingi wa

ushirika sio kupitia dhehebu au mashirika, ni kwa Damu ya Yesu Kristo ambapo Damu hutusafisha na dhambi zetu na kutuleta mahali pamoja.

97 Sasa, Mfarisayo Wake, Msadukayo, ama yeyote yule, alikuwa na haki ya ushirika huo, bali asingeweza kuwa kwa sababu alikuwa Mfarisayo, kwa sababu alikuwa ni Msadukayo, aliingia katika ushirika huo kwa kuja chini ya damu. Huyu hapa anaelekea ukutani sasa, anatambua nyakati hizi saba.

Katika miaka elfu sita, Mungu aliujenga ulimwengu; elfu saba ni mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu, raha Yake.

98 Sasa, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, miaka elfu mbili, jambo fulani limetukia: Miaka elfu mbili ya kwanza, Nuhu alijenga safina; elfu mbili ya pili, Kristo akaja; 1960, inakaribia mwisho. Mnaona?

99 Na sasa ya saba, kama vile Mungu alivyofanya kazi na kuujenga ulimwengu katika siku sita, miaka elfu sita, ambayo tunajua Maandiko yanasema ya kwamba siku moja ni miaka elfu Mbinguni, nayo ile elfu ya saba, Kanisa limeshindana na dhambi kwa miaka elfu sita, halafu ile elfu ya saba ni ule Utawala wa Miaka Elfu na kumbukumbu kwa viumbe vyote, ya kwamba Mungu amelikomboa Kanisa Lake.

100 Alimwambia Adamu, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Anapomwacha mwanadamu aishi miaka elfu moja, ni mfano na kumbukumbu kwamba kamwe hatamwangamiza mwanadamu tena, wala hakutakuwako na dhambi tena, kwamba amerudi katika ushirika pamoja na Mungu, Milele. Amina. Hiyo ni kweli. Tuko moja kwa moja kwenye jambo hilo sasa.

101 Sasa, tunakuja mlangoni, tukiitambua ile damu. Ndipo unapokuja chini ya damu, unaingia madhabahuni, umefunikwa na uwepo wa Patakatifu pa patakatifu, Utukufu wa Shekina, yote katika madhabahu. Wakati lilipowekwa wakfu, chumba chote kilijaa moshi, wakati Sulemani alipoliweka wakfu lile hekalu.

102 Kwanza: Maji ya farakano, bado si sawa, kuitambua ile Damu, uko njiani, uko mlangoni. Inayofuata: kuingia Patakatifu pa patakatifu. Niseme nini juu ya jambo hilo? Luther, chini ya kuhesabiwa haki, akiliamini Neno; Wesley, chini ya utakaso, mlangoni; Pentekoste, katika Roho Mtakatifu, na ushirika, na Utukufu wa Shekina.

103 Huwezi kusimama nje ya mlango, uangalie ndani, useme, "Hao watu wana shida gani?" Huna budi kuingia chini ya Damu hiyo na kuingia katika Utukufu wa Shekina, ndipo nguvu za Mungu zinaanza kushuka, ndipo unaanza kuona kile kilichotukia. Utaninii . . . Kama nilivyosema hivi majuzi usiku kuhusu kuingia majini, huna budi kuingia ndani yake kabla ya kujua yote yanahusu nini.

104 Sasa, hapo, kama tu vile unavyoishi maisha yako, unaishi jambo lile lile. Na kama...Unaishi tu katika nyumba ya vyumba vitatu; Mungu aliishi katika nyumba ya vyumba vitatu: Nafsi, mwili, na Roho; Mungu aliishi katika—katika nyumba ya vyumba vitatu, ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; nawe unaishi katika nyumba ya vyumba vitatu; Roho huja kupitia nyumba ya vyumba vitatu: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

105 Nawe unaishi katika nyumba ya vyumba vitatu, kawaida. Kwanza, una jikoni, kinachofuata ni sebule, kingine ulicho nacho ni chumba cha kulala. Angalieni hao mume na mke vijana, kabla hawajakamilika katika upendo huo wa fileo, ama upendo wa fileo, jambo la kwanza ni lipi? Ni kwamba wanaahidiana. Wanafunga ndoa, na wanaishi katika nyumba hii ya vyumba vitatu.

106 Sasa, huenda ukawa na vyumba viwili vya kulala, huenda ukawa na chu—chumba cha ziada cha kulia chakula, bali ungali tu unaishi katika vyumba vitatu. Nawe unaishi katika mwili huu, kama nyumba ya vyumba vitatu: nafsi, mwili, roho. Kila kitu, ambacho wewe, popote unapotaka kupitia, maumbile ama chochote kile, chote kinakuja kwenye hizo tatu, Mungu amekamilika katika hiyo namba, tatu.

107 Sasa, angalieni jambo hili sasa wakati akija, wanakuja jikoni. Nini? Kula, unakula jikoni, hicho ndicho chako cha kwanza. Halafu unaingia chumbani kuzungumzia mambo, kutambuana, kufanya maungamo yenu yote. Lakini basi, mnapoingia katika chumba cha kulala, hapo ndipo maisha yenu ya ndoa yanakamilika. Uko tayari basi, uhai uko tayari, kwa ajili ya watoto, na kadhalika.

108 Hivyo ndivyo Kanisa lilivyo, linapokuja kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, kuingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, Kanisa liko katika utungu wa kuzaa wakati huo, kuwazaa watoto wadogo, wakilia, "Mungu wangu, Mungu wangu!" Mnaona? "Abba, Baba." Mnaona?

109 Hivyo ndivyo tunavyopitia kwenye elementi hizo kwenda Mbele za Mungu kwa ajili ya ushirika. Ushirika hutambuliwa tu chini ya Damu.

110 Mtu aliye nje, akisimama katika kuhesabiwa haki, anaweza kusikia Neno, huenda akawa msemaji wa namna yoyote ambaye angeweza kulielezea Neno hilo kwa njia ambazo—ambazo jamaa huyo mwingine hajui lolote kuzihusu, lakini hata hivyo, kama hajapitia kwenye elementi hizo chini ya Damu hata kwenye ushirika na Utukufu wa Shekina, hajui tunachozungumzia.

111 Lakini hapa, ambapo sote tumempokea Roho Mtakatifu, sisi sote ni mmoja kwa kuwa sote tumenyweshwa Roho yule yule, kama sisi ni Umoja, Uwili, Utatu, Utano, Assemblies, Pentekostal Holiness, lolote lile, sisi sote ni mmoja katika

Kristo Yesu, "Kwa kuwa katika Roho mmoja sote tumebatizwa," tukiisha kutakaswa, kuwa Roho mmoja.

112 Kuhesabiwa haki, ni Maji ya farakano; utakaso, kutakasa nafsi zetu, ndipo tutakapoingia katika Patakatifu pa patakatifu palipo na Utukufu wa Shekina, kwa Roho huyo mmoja tunabatizwa kuwa Mwili huo mmoja na kufanya ushirika pamoja na Mungu. Amina. Mungu amerudi kama alivyokuwa katika bustani ya Edeni, akishirikiana na nafsi zetu, akizungumza nasi.

113 Si ajabu watu wanasimama nje wakiwa na elimu ya kiakili, wakijaribu kujua kile watu hawa wanachofanya mle ndani. Kamwe hutaweza kufanya hivyo kwa Maji ya farakano pekee, huna budi kutambua ya kwamba mnyama huyo, ama, Kitu kile kilichokufa kwa ajili yako, kweli kilikuwa na mwili kilichoutoa, alikuwa na Damu ambayo alimwaga, ana Uhai unaokurudia, Yesu ndiye yale Maji ya farakano. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Huu ni Mungu, Ujumbe wa Mungu kwako kwamba Yesu alikufa kwa ajili yako, Maji ya farakano.

114 Utakaso ndio unaotusafisha. Na Roho Mtakatifu aliyetoka Kwake, sababu ya wanyama kutoweza kuwapa Roho Mtakatifu, ni kwa sababu mnyama, uhai uliokuwa ndani ya mnyama, wakati uhai huo ulipotolewa, ulikuwa ni uhai wa mnyama, haungepatana na uhai wa mwanadamu, kwa sababu mnyama hana nafsi.

115 Lakini wakati Yesu alipokufa, basi Yeye hakuwa mwanadamu tu, bali alikuwa ni Mungu na mwanadamu, Mungu aliyefichwa ndani ya mwanadamu, na wakati Chembe hiyo ilipovunjwa, Mungu aliachiliwa tena apate kurudi kupitia Damu iliyomwagika kutakasa na kuishi katika kila chombo ambacho kingethubutu kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ndiyo sababu tuna ushirika huo, huo ndio unaofanya kitu halisi, ni kitu kama hicho.

116 Mungu ana maandalizi. Hiyo ndiyo sababu watu hawa wana furaha, hilo ndilo linalowafanya watu jinsi walivyo, kwa sababu wameingia katika mahali hapa Patakatifu pa patakatifu, wako chini ya nguvu za Mungu. Wana—wanatembea katika—katika uzuri wa kufufuka Kwake, mbona bila shaka, Mungu huyo aliyefufuka, akiishi katika Patakatifu hapa pa patakatifu. Hebu niwaambie yaliyotukia, waangalieni wakinyooka, maskini watu waliokufa ambao hawangeweza kufanya lolote, angalieni yanayowapata.

117 Vema, siku moja waliiacha fimbo ya Haruni mle ndani. Jamani, jamani! Aliporudi mwaka uliofuata kuichukua, ilikuwa na maua juu yake, na tayari ina uhai ndani yake, na ilikuwa na majani juu yake, na maua juu yake.

118 Nanyi chukueni uhai wowote wa kale, uliokufa na kuuweka katika Patakatifu pa patakatifu kwa muda, na kuuacha upitie kwenye mchakato huo wa Damu, maji, na utakaso, kisha uingie katika Patakatifu pa patakatifu, utachanua, kama yeye ndiye mwanamke mchafu kuliko wote katika mji huu, ama mcheza kamari mbaya kuliko wote aliyeko, mtamsikia akisimama kwenye kiamshakinywa asubuhi fulani na kutoa ushuhuda ambao utatikisa viezeko kutoka juu ya nyumba hapa. Kwa nini? Ni kwa sababu amekuja katika ushirika, maisha hayo yaliyokufa yamefanywa upya tena.

119 Sasa, unaweza kuchukua fimbo ya Haruni, na kuiweka juu ya—ya Maji ya farakano, haingefanya hivyo; iweke juu ya—juu ya damu, haingefanya hivyo, lakini baada ya kupitia kwenye damu ikaingia katika Patakatifu pa patakatifu, hapo ndipo ushirika unapokuja, hapo ndipo uhai huja, uhai huja kwa Roho. Amina.

120 Ndipo Mungu akafanya tiba kwa ajili ya jambo hilo. Katika kufunga huenda nikasema hivi: Katika bustani ya Edeni, wakati Mungu alipoona ya kwamba watoto Wake walikuwa wametenda dhambi na walikuwa wamemwacha, Mungu Mwenyewe, Ambaye ndiye Hakimu mkuu, alifanya upatanisho kusudi aweze kurejesha ushirika huo kwa viumbe Vyake kwa damu iliyomwagika ya mnyama. Na hiyo damu iliyomwagika ilidumu kwa miaka mingi chini ya . . . ikinena juu ya kuja kwa Kristo.

121 Lakini siku moja, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, Mungu alifanya ushirika mkamilifu kurudisha, si kuingia katika maskani, kama alivyosema, iliyofanywa kwa mikono, ambamo kuhani alienda kila mwaka akiwa na damu kwa ajili ya watu na kwa ajili yake mwenyewe, lakini katika siku hii, Yesu, mara moja tu, alinunua ushirika wa Milele kwa ajili yetu. Si kila mwaka kufanya ukumbusho, arudi na kusema, "Vema, nimetenda dhambi, nimefanya *hivi*, nami nilienda na kufanya *hivi*," na kutoa mwana-kondoo mwingine, na—na jambo lingine.

122 Yesu, mara moja tu, wakati mmoja amewakamilisha, milele, wale ambao wamekuja katika ushirika huo, pamoja na baraka ya Milele, ushirika wa Milele, pamoja na Uwepo wa Milele wa Mungu, kwa—kwa nguvu za Roho Mtakatifu, si kwa mfano huko nje, ama katika neno fulani, ama katika theolojia fulani, bali Roho Mtakatifu ndani *yako*. Nguvu za Mungu zilizomfufua Kristo kutoka kaburini zinafanywa hai ndani yako, nawe ni kiumbe kipya, basi wewe ni mwana na binti wa Mungu. Loo, ndugu, hmm! Jambo ndilo hilo. Loo, inahitaji Da—Damu ya Yesu Kristo kuchochea, inahitaji nguvu za . . . Uhai uliokuwa katika hiyo Damu.

123 Mnaona, kuna elementi ya Uhai katika Damu. Uhai uko kwenye seli ya damu. Uhai hutokana na jinsia ya kiume, si kwa mwanamke, mwanamke hawezi kutoa uhai, maana yeye

ndiye yai. Lakini yeye hutoa yai, lakini mwanamume hutoa seli zazi. Chembechembe ya uhai hutoka kwa mwanamume, kwa sababu iko katika seli ya damu, na katika chembe hiyo ya damu kuna uhai. Na katika Seli ya Damu, katika hali. . .kwa Yesu hakukuwa na tendo la kujuana kimwili la mwanamume, bali nguvu za uumbaji za Mungu, ziliumba Seli ya Damu, katika tumbo la uzazi la Mariamu, kwa yai hilo lililomzaa Mwana wa Mungu, ambayo ilikuwa ni maskani ambayo Mungu aliishi ndani yake Mwenyewe. Loo, ndugu!

124 Moja ya siku hizi ninataka kuwahubiria *Ile Ishara Kuu*. Kila mtu anataka ishara, naye Mungu akampa ishara kuu, nayo hiyo ishara kuu ilikuwa, "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana," ile ishara kuu, moja ambayo ilikuwa iwe daima kumbukumbu ya kwamba Mungu Mwenyewe, alijifanyia Mwenyewe mwili kisha akashuka. Alijibadilisha Mwenyewe kutoka kwa Mungu apate kuwa wa ukoo wetu. Haleluya! Mungu alifanyika mwanadamu, akatandaza maskani Yake apate kuishi pamoja nasi.

125 Vema, nena kuhusu ishara kuu! Yeye angeweza kuja kama Malaika kama angalitaka, angeweza kuja kama mtu mzima kabisa, bali Mtoto mchanga, juu ya lundo la samadi, akilia. Ee Mungu! Nena kuhusu Ishara kuu! Hiyo ni ishara kuu halisi, Mtoto mchanga, Yehova akilia kama Mtoto mchanga, ishara kuu. Loo, jamani!

126 Halafu ati watu wanasema Yeye ni nabii tu. Loo, jamani! Ishara kuu: Yehova kama Mvulana, akicheza, Yehova, Mtu anayefanya kazi kwa bidii kwenye duka la seremala, Yehova, Mwenyewe aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, akatandaza hema Lake huku chini, akajifanyia Mwenyewe mwili kuishi ndani yake, apate kuwa na Seli ya Damu, ili kwamba Seli hiyo ya Damu iweze kuvunjwa. Haleluya! Huyo alikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, anayetuletea ukombozi wa Milele. Biblia ilisema hivyo hapa, alitununulia ukombozi wa Milele. Tumenunuliwa kwa Damu ya thamani ya Yesu Kristo, ambayo imetupa Uzima wa Milele. Alifanyaje jambo hilo? Sijui.

127 Mnajua ibilisi daima alichungulia ndani apate kujua Yeye alikuwa ni nani. Siku moja walisema, "Kama Yeye ni Masihi, Yeye ata—Yeye hakika atafanya ishara fulani ya ajabu."

128 Akasema, "Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate." Masihi ni mtenda miujiza, angali bado, daima amekuwa. Bila shaka. *Masihi* alikuwa "Mtiwa mafuta."

129 Aliyetiwa mafuta leo hii ni Kanisa la Kimasihi, Kanisa hili, Kanisa hili la aliyezaliwa upya. Kanisa hili limekuja kupitia maji, "Imani huja kwa kusikia"; kupitia Damu, uhai uliotakaswa; kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ndiye Yule aliyetiwa mafuta, Kanisa la Kimasihi. Utukufu!

130 Mbona, Kanisa la Masihi litakuwa na ishara za Masihi ndani Yake. Haleluya! Hakika, kwa sababu ni Kanisa la Kimasihi, Hilo ni Kanisa la Masihi. Amina. *Brrrrr*! Hilo linanifanya nijisikie vizuri kama jamaa yule alivyojisikia muda mfupi uliopita. Naam, bwana. Kanisa la Kimasihi lenye nguvu za Kimasihi, pamoja na ishara za Masihi. Amina. Haya basi. Hapo ndipo unapofanyia ushirika. Loo, hakuna kitu kama hicho, ni kamilifu.

131 Sasa, wazia juu ya Yehova akifanya jambo kama hilo. Huyu hapa, ibilisi akamtazama, akasema, "Nashangaa kama huyo kweli ni Mwana wa Mungu? Sijui, hivi huyo ni nabii wa kawaida tu, ama huyo ni Mwana wa Mungu?" Akasema, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate." Mnaona, kweli alikuwa kijana mwenye akili. Yeye—yeye—yeye kweli alijua kile alichokuwa anazungumzia.

132 Lakini Yesu akasema, "Imeandikwa!"

133 Sasa, alimpandisha juu na kuendelea kumjaribu apate kujua. Siku moja akampeleka katika—katika nyua za mataifa, naye akaendelea kushangaa, "Huyo angeweza kuwa?" Mnaona?

134 Mungu kweli alimpumbaza Shetani wakati ile Ishara kuu ilipokuja, hakujua Yeye alikuwa ni nini. "Yehova angewezaje kuzaliwa katika hori? Yehova angewezaje kulia kama mtoto mchanga na kuvaa nguo za kitoto." Mbona hakika. Alikwepa . . . Yesu alikuwa dhabihu iliyojitolea ya Mungu.

135 Nafikiri Maandiko matamu sana yaliyopo katika Biblia nzima ni Maandiko haya: "Baba, najitakasa Mwenyewe kwa ajili yao." Yeye alikuwa ni mwanamume, angeweza kuwa na mke, Yeye alikuwa mwanamume. Angeweza kuwa na makazi, mahali pa kulaza kichwa Chake, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa na haki za hayo, alikuwa mwanamume. Angeweza kuwa na nguo nzuri, Yeye alikuwa mwanamume. Lakini alisema nini, "Baba, najitakasa Mwenyewe kwa ajili yao."

136 Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiwafundisha wanafunzi kumi na wawili ambao walikuwa wanaenda kuihubiri Injili ulimwenguni kote, aliweka mfano. Nanyi ndugu, kama wahudumu, nawaambia inatufaidi, tusiwe na mali nyingi sana za ulimwengu na kadhalika zikining'inia kwetu, ninyi wahubiri ninazungumza nanyi, jitakase kwa ajili ya hao ambao utawaongoza. Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ni maisha makamilifu yaliyowekwa wakfu, yaliyotakaswa, ya wahudumu wanaotembea kwa unyofu mbele za Mungu, wasiojihusisha na mambo ya ulimwengu, wanaokaa mbali nayo. "Baba, najitakasa Mwenyewe kwa ajili yao." Kwa kuwa . . . Si kwa sababu ilimbidi kufanya jambo hilo, bali alilifanya kwa ajili yao.

137 Sasa, wakati Warumi walipomfunga kitambaa usoni Mwake, nao walijua angeweza kuona maono, basi walimpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, "Tuambie, ni nani aliyekupiga. Kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga. Sasa, tutakuamini."

138 "Bali hakufunua kinywa Chake." Mnaona hekima ya Mungu? Huyo angelikuwa ni nabii wa kawaida angeghadhabika akerwe sana pale, ama kitu fulani, lakini Yeye alikuwa ni Mungu, Alijua la kufanya, alijua huyo alikuwa ni nani ndani ya watu hao.

139 Alipofika kwenye, alipoanza kupanda msalabani, wao walisema, "Aliwaokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe." Hiyo ilikuwa ndiyo sifa kuu sana aliyowahi kupewa. Mbona, kama angalijiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine, bali Yeye—Yeye alijitoa Mwenyewe kusudi aweze kuwaokoa wengine na kufanya maandalizi. Mungu wa Utukufu, akimtukuza Mungu katika Utukufu, akimtukuza Mungu wa Utukufu. Amina. Nena kuhusu Ishara kuu na njia iliyowekwa, mahali ambapo tungefanya ushirika!

140 Hebu tumwangalie kwa dakika chache. Ulimwengu uko gizani, kanisa katika msimamo wake wa kiakili limeanguka chini, limeporomoka, taifa lenyewe liko kifungoni. Ni asubuhi yenye giza, kwanza, jua linachomoza vizuri, ndipo moshi unaanza kukusanyika duniani. Tunasimama katika chumba cha juu huko Yerusalemu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, na hebu tufanye safari ndogo sasa, na tuangalie mahali ushirika wetu, kilichotukia, sababu ya sisi kuweza kufanya ushirika. Hebu tuangalie tu kwa dakika chache tuone kama si juu ya msingi wa damu iliyomwagika.

141 Ninamwona, ninasikia kelele nje ya dirisha. Ni kitu gani? Ah, baadhi yao wakisema, "Kwani amefanya nini?" Ninamwona maskini mwanamke mmoja akikimbia mbele akisema, "Kwani amefanya nini? Amewaponya tu wagonjwa, na kuwafariji maskini, na kuleta Uzima, matumaini ya Uzima, kwetu."

Mtu fulani anampiga kofi atoke barabarani, kasema, "Je, ungemsikia badala ya mchungaji wako mwenyewe, kasisi wako? Mwondoeni!"

Mtu mwingine anasimama, asema, "Nilikuwa na mguu uliolemaa, Naye akaniponya."

"Mpelekeni kwenye mti wa kunyongwa." Mnaona? Loo, ni wakati wa jinsi gani!

142 Ninasikiliza kitu fulani kikigongagonga, hebu tufungue pazia, tuangalie nje. Ninaona, akishuka kuja barabarani, tamasha ambayo ingevunja moyo wa mtu mgumu kama chuma, Mtu ambaye alikuwa—ambaye hakuwa na hatia ya dhambi yoyote, bali hata hivyo amejitwika dhambi ya ulimwengu wote juu Yake. Hakujua dhambi kamwe, kamwe hakumchukiza Mungu hata wakati mmoja, Baba Yake. Kamwe hapakuwapo na wakati mmoja ambapo Yeye alifanya jambo lolote baya, alikuwa ndiye Mtu mkamilifu, na wa pekee aliye mkamilifu ulimwenguni, nalo kanisa lisilo kamilifu likamhukumia kifo. Nena kuhusu mahali fulani!

143 Walitaka madhehebu yao wenyewe, ushirika wao wenyewe, na kadhalika. Lakini Mungu alikuwa akifanya njia kwa ajili ya mwaminio wa kweli, kwa ajili ya waaminio wanyenyekevu kweli, waaminifu. Nilisema jana usiku, kila wakati ibilisi anapotoa Goliathi, Mungu ana Daudi mahali fulani. Kwa hiyo, ninii tu—sikuzote kumbukeni tu hilo.

144 Sasa, Mungu alikuwa akiandaa njia kwa ajili ya mwaminio wa kweli, kama vile Yesu alivyosema, "Wakati unakuja ambapo. . .Mungu ni Roho naye ataninii. . .Yeye huwatafuta wale watakaomwabudu katika Roho na katika kweli.

145 Ninausikia ukigongagonga, ninaangalia chini na kumwona maskini Jamaa, dhaifu, Ana maskini joho jeupe juu ya mabega Yake, limefumwa kote bila mshono. Anaposhuka akiuburuta msalaba, unagongagonga barabarani, ukigonga kichwa Chake, miiba, Damu ikitiririka usoni Mwake, anapoanza kupanda kilima.

146 Ninaona alama ndogo nyekundu kwenye koti Lake. Swali ni: Hizo ni nini? Ni nini alama hizo ndogo nyekundu nyuma ya koti Lake anapopanda kilima? Kadiri anavyoenda mbali, ndivyo alama hizo ndogo zinavyozidi kuangaza, na ndivyo zinavyozidi kuenea, zikienea zaidi, zaidi. Na muda si muda mwajua, zote zinakuwa doa moja kubwa mno, jekundu, nayo Damu inapigapiga miguuni namna *hiyo*. [Ndugu Branham anapigapiga mikono yake pamoja—Mh.]

147 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akifanya maandalizi kwa ajili ya ushirika, Mungu akifanya njia tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ushirika, kwamba tungeweza kuja hapa chini ya nguvu za Roho Mtakatifu na kufurahia baraka za kiroho, tukiuacha ulimwengu nje. Hawajui lolote kutuhusu, hawajui lolote kuhusu ibada yetu, hawajui chochote kumhusu Mungu wetu, wako tu huko nje katika namna fulani ya. . .Wanaenda kanisani, loo hakika! Ni kile nilichokuwa nikizungumzia jana usiku. Usijaribu kuwa kama wao, njoo chini ya Damu ya ushirika. Na tuje pamoja, na kuketi katika ulimwengu wa Roho.

148 Ninaona, anapoyumbayumba na kuanguka, na kusimama kwa miguu Yake, nao wangempiga mijeledi, na kumpiga, na kumpiga kofi, na kumtemea mate, na uso umejaa mate, na. . . Ni aibu jinsi gani! Laiti ungeweza tu kuona jambo hilo na kujua ya kwamba dhambi zako ndizo zilizosababisha hilo! Huyo alikuwa ni Yeye akichukua adhabu yako, hiyo ilikuwa ni Bampa iliyokuwa imesimama kati yako na Mungu sasa hivi. Mungu angekuua dakika hii, maana Yeye hawezi kuangalia udhalimu, bali kulikuwako na upatanisho uliofanywa kwa ajili ya dhambi zetu.

149 Damu ilikuwa ikiosha ardhi, tangu Habili asiye na hatia moja kwa moja hata—hata wakati huo. Kupitia kwa mwana-kondoo, baada ya mwana-kondoo, baada ya mwana-kondoo,

na ndama baada ya ndama baada ya ndama, lakini sasa Neno lilikuwa likidhihirishwa. Neno lilikuwa linaenda kufanyika Roho, Neno lilikuwa linaenda kukaa miongoni mwetu, Neno linaenda kuwa ndani yetu, "Nitaandika sheria Zangu katika vibao vya mioyo yao." Jambo fulani lilikuwa likitukia.

150 Sasa angalieni, akipanda barabarani, hapo akaja nyuki. Ibilisi akasema, "Unajua nini? Mtu mwenye fedheha hivyo asingeweza kuwa Mungu. Hivyo tu, isingewezekana."

151 Hivyo ndivyo wanavyowazia siku hizi, "Watu wangewezaje kupiga mayowe, na—na kujaribu kupayuka-payuka katika lugha nyingine, na wangeenda huko nje na kupiga makelele, na—na wanawake, wanawake warembo wangejinyima wasiwaonyeshe watu miili yao, jambo ambalo walifanyiwa, na mambo haya mengine yote, na kama vile, wangejifunikaje namna hiyo, na wasichana wadogo, warembo bila ya kujipodoa, na kadhalika, waketi tu, na mambo kama hayo?" Mnaona, hawalipati. Wanasema, "Imekuwaje?"

152 Hivyo ndivyo ibilisi alivyosema kuhusu Mtu huyu, "Angewezaje kuaibishwa?"

153 Mchukue msichana kutoka kwenye roki, acha aingie kwenye ushirika huu, atajisafisha upesi sana, ataacha nywele hizo zikue, na kuvaa mavazi mazuri, ya heshima, avue maskini hizo kaptura na suruali ndefu, naye ni tofauti. Kasema, "Ilikuwaje kwa mwanamke yule?"

154 Hilo ndilo jambo lile lile alilowazia ibilisi, "Loo, hilo haliwezi kuwa sahihi," mnaona, "hilo haliwezi kuwa sahihi, yeye si Mwana wa Mungu." Kwa hiyo akasema, "Njoo ewe mauti, shuka uende kule chini ukamkamate, yeye si Mwana wa Mungu, la sivyo asingekuwa katika fedheha hivyo." Mnaona?

155 Kile alichowazia kilikuwa ni fedheha, bali alikuwa anaichukua ile shutuma. Natumaini mnaona kile ninachozungumzia. Huenda nisiweze kulifanya dhahiri vya kutosha, mnaona. Yeye alikuwa akichukua shutuma yako.

156 Ndipo wakati akipanda kile kilima, ibilisi akasema, "Njoo, ewe mauti, shuka ukamchome na kumwua sasa." Vema. Ibilisi akatoka, ule mwiba wa mauti ukashuka, ukaanza kumzunguka.

157 Unajua, kila mtu anaogopa uchungu huo wa mauti, maana ni mbaya sana, unaona, uchungu wa mauti. Mmewasikia wakipiga makelele, na kulia, na kupiga mayowe, na, wapate rehema. Nina kitabu juu ya maneno ya mwisho ya watu mashuhuri, na karibu nusu yake yamewekwa kwenye maneno ya mwisho ya watu mashuhuri wa ulimwengu, wafalme na malkia waliokufa bila Mungu. Malkia mmoja alisema, ninaamini malkia wa mahali fulani, Uingereza, ama mahali fulani, alisema, "Ningeutoa ufalme wangu na yote yaliyokuwa ndani yake kama ningepata dakika tano zaidi za maisha nipate kutubu." Mnaona? Mnaona? Asingeweza kufanya hivyo. Mnaona?

158 Halafu nimekuwa na maisha ya watu mashuhuri kama Dwight Moody, na hao wengine, wakati alipoinuka, kasema, “Je, haya ni mauti?” Kasema, “Hii ndiyo siku yangu ya kutawazwa.” Mnaona? Hakika.

159 Nina maisha ya Paul Rader, ambaye ulinenwa, tuliongoka katika maskani yake, Paul, alipokuwa akifa, alimwita ndugu yake Luke, aliyekuwa kwenye chumba cha pili, akasema, “Yuko wapi Luke?” Naye Luke alikuwa kwenye chumba kingine. Akasema. . . Kwa namna fulani Yeye na Paul waliambatana, kama vile mimi na Billy tulivyo pamoja. Basi a—akasema, “Luke, tumetoka mbali pamoja, sivyo, Ndugu?” Kasema, “Tumepitia vita vingi vikali pamoja.”

Luke akasema, “Hiyo ni kweli, Paul.”

160 Paul akasema, “Liwazie: Dakika tano kuanzia sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

161 Nikamkumbatia, nikambusu, tukaondoka, nami nikaenda huku nikilia. Saa chache tangu wakati huo, alisimama chumbani, akasema, “Vema, kama yule pale si Ndugu *Nanii*, aliyeongoka katika mkutano wangu!” Alikufa, alikuwa amekufa miaka hamsini, akampa mkono, ndipo akasimama sakafuni, akipeana mikono na watakatifu wa Mungu ambao tayari wameenda Mbinguni, waongofu wake wa miaka hamsini iliyopita. Sijui, kama hakuingia Mahali pale nilipokuwa hivi majuzi asubuhi, na kuwaona huko, akiwapa mikono namna hiyo.

> Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha
> Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
> Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
> Kumbukumbu za kudumu;
>
> Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
> Huku akisafiri kwenye barabara kuu ya maisha,
> Ndugu mpweke na aliyeharibikiwa meli,
> Akiona, atajipa moyo tena.

Hiyo ni kweli.

162 Sasa, nyuki huyu alisema, “Unajua nini?” Mauti haya yalisema, “Yeye ni mwanadamu tu, hamna lingine kwake. Yeye ni nabii wa kawaida tu, la sivyo angefanya jambo fulani kulihusu huko chini. Mungu asingekufa namna hiyo, kwa hiyo nitamuuma.” Naye akauchomeka mwiba huo ndani Yake msalabani.

163 Loo, ndugu, hivi uliwahi kujua, wakati nyuki anapochomeka mwiba wake, unajua kinachotukia? Kama kweli ameuchomeka ndani sana, yeye hana mwiba tena. Basi wakati ule mwiba

wa mauti ulipochomekwa katika mwili wa Mungu, huo mwiba uling'oka. Hiyo ni kweli.

164 Kwa hiyo leo, hatuna uchungu wowote wa mauti. Anaweza kulia na kupiga kelele, bali tunaweza kusimama kama Paulo, aliye chini ya ushirika huu, "Ee mauti, u wapi mwiba wako? Ewe kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

165 Hapo ndipo mauti yalipomezwa katika ushindi, wakati nyuki alipopoteza mwiba wake. Nyuki wa mauti alipoteza mwiba wake alipomwuma Mungu Mwenyezi aliyedhihirishwa katika mwili pale Kalvari, leo hana mwiba tena.

166 Hivi hamna furaha kuwa chini ya ushirika huu? Hivi hamna furaha mlisikia Neno? Imani huja kwa kusikia, kuchukua imani rahisi na kuitumia, kutwaa mwerezi wa msalaba, na kutakaswa tuyaache mambo yote ya ulimwengu, kisha tuingie kwa sufu nyekundu, sufu iliyochovywa kwenye rangi ambayo ilifanya sufu iwe nyekundu kwa damu ya mnyama, na hivi hii sufu, sisi wenyewe tukitiwa rangi. Loo, jamani!

167 Nilikuwa mwenye ukoma wakati mmoja, nimetiwa tu madoa ya dhambi kadiri nilivyoweza kuwa, lakini Yeye akanipeleka kwenye pipa la Damu Yake Mwenyewe, naye akanitia rangi mle ndani. Ndipo basi niko ndani ya maskani ya Mungu sasa, pamoja na neema chini ya ushirika.

168 Wakati mmoja ningesimama mtaani, baba yangu mwuzaji pombe haramu na kila kitu, hakuna mtu, bila nguo za kuvaa, na nywele zikining'inia shingoni mwangu, na sijavaa viatu, miguu yangu ardhini, na watu hata wasingezungumza nami, hata kijana mwanamume, kwa sababu familia ilikuwa na jina baya sana, kurushiana risasi, kupigana, kuua, na kila kitu. Mtu fulani angekuwa akizungumza nami, nao wangeondoka, wakimwona mtu mwingine akija, maana hawakutaka kuwa wamesimama wakizungumza nami, wakutwe mtaani. Nikaendelea kushikilia, "Kuna Kitu fulani kikuu kuliko hiki. Kuna Kitu fulani, mahali fulani."

169 Nilienda kwenye ile beseni nikatiwa rangi katika Damu ya Bwana Yesu. Na hivi majuzi mke wangu alisema ninapoenda nyumbani inanibidi kwenda mahali fulani kisiri na kuingia mwituni kuwazuia watu, nipate dakika chache za kupumzika.

170 Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Ati utu? Sina wowote. Kitu gani? Elimu? Sina yoyote. Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Damu ya thamani ya Yesu Kristo ambayo imenisafisha na dhambi, na kunitakasa, na kuitia rangi nafsi yangu katika wema Wake na rehema Zake, na sasa niko chini ya ushirika pamoja na makumi ya mamilioni ya watakatifu wa Mungu kote ulimwenguni, huo ndio ushirika halisi, wa kweli. Nina furaha sana mimi ni mmoja wao. Nanyi je?

171 Nitawaimbia wimbo mmoja. Ninajua utawashtua, lakini nitawaimbia mmoja. Sijui kama ninaweza ama siwezi lakini nitajaribu.

> Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha juu,
> Wote wakiomba katika Jina Lake,
> Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
> Na nguvu zikaja kwa ajili ya huduma;
> Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
> Atakufanyia vivyo hivyo,
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
>
> Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)
> Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
>
> Njoo, ndugu yangu, utafute baraka hii
> Itakayousafisha moyo wako na dhambi,
> Itakayofanya kengele za shangwe ziaze kulia
> Na itaiwasha moto nafsi yako;
> Loo, inawaka sasa moyoni mwangu,
> Loo, utukufu kwa Jina Lake,
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

172 Hivi huna furaha asubuhi ya leo, wewe ni mmoja wao? Ninakumbuka nikitembea barabarani, mnajua ile hadithi yangu ndogo kuhusu yule mwanamke mweusi huko Memphis, wakati huo. Jinsi ambavyo nilikuwa nikishuka mtaani, nikiuvumisha wimbo huo, naye alikuwa amesimama pale, akiningojea. Bwana alimponya mvulana wake. Naam, bwana.

> Loo, watu hawa huenda wasijifunze kuwa (Hawana elimu.),
> Au kujivunia sifa za ulimwengu,
> Wote wameipokea Pentekoste yao,
> Kwa imani katika Jina la Yesu;
> Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na kwa upana,
> Nguvu Zake zingali ni zile zile,
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

173 Loo, jamani! Nililipataje? Kwa ushirika wa Damu. Nilikuja kutoka kwenye kichochoro, nipate kuwa ndugu yenu, kushirikiana nanyi katika mambo mema ya Mungu chini ya Damu iliyomwagika, kwa ajili ya ushirika wa watakatifu wanaoabudu pamoja na Mungu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

174 Kunaweza kuwa, kwa bahati, mtu hapa ambaye hajaingia katika ushirika huo? Hujui Utukufu wa Shekina ni nini, unasema, "Ndugu Branham, mimi ni Mkristo, niliungama."

Hilo ni sawa. Umepitia kwenye Maji ya farakano.

175 "Loo, vema, Ndugu Branham, ni—nimetakaswa. Sivuti sigara wala kunywa pombe na . . . "

176 Hilo ni sawa kabisa, ndugu yangu, lakini je, umeingia katika ushirika, bado, ambapo Mungu anakutana nawe chini ya Damu iliyomwagika? Ukiisha kuja chini ya Damu iliyomwagika, Uhai katika Damu hiyo unarudi katika umbo la Roho Mtakatifu, ambaye ni Kristo katika Roho, kushiriki pamoja na watoto Wake.

177 Kama hujaninii, unataka kukumbukwa katika maombi, waweza kuinua mkono wako, useme, "Nikumbuke." Mungu akubariki, mama. Loo, jamani! Mikono minane ama kumi, kumi na mitano.

Na tuombe.

178 Bwana, loo saa imechelewa. Na, lakini, Ee Mungu, kweli hii ya thamani, mahali hapa pa ushirika, hapa chini ya Damu ya Bwana Yesu, jinsi nilivyo na furaha!

> Neema ya ajabu! (akasema mshairi,) jinsi inavyosikika tamu,
> Ambayo ilimwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, lakini sasa ninaona.

179 Baba Mungu, nisaidie kujiweka nimetakaswa, mdogo, kamwe nisiwe mkubwa, unijalie tu niwe jinsi Wewe ungetaka niwe, kusudi iweze kumpata maskini ndugu ambaye—ambaye hana nafasi, kwamba labda anaweza kuona ya kwamba—ya kwamba neema Yako inatosha kwa mambo yote. Na iwe ni kumbukumbu, Bwana, inayodumu nyakati zote.

180 Maisha yangu yatakapokwisha, kama Ndugu Carlson alivyosema, mimi na Ndugu Roberts, na sisi sote hatuna budi kuondoka siku moja, lakini Mungu, wakati nikiwa hapa, jalia nikumbuke lile shimo nilimochongewa, hebu nikumbuke ile Damu ya thamani siku zote za maisha yangu, nijiweke mdogo, kwamba maskini ndugu huyo, ambaye—ambaye anaweza kuwazia ya kwamba Mungu anaweza tu kuwashughulikia wa tabaka la juu, matajiri, amjalie kuona kwamba Mungu . . . hebu nifanye alama ya kudumu mahali fulani, Bwana, ambayo ingemwongoza ndugu huyu kwenye mahali pa ushirika. Tujalie, Bwana.

181 Bariki mikono hii iliyoinuliwa, wako humu ndani wakitafuta na kutamani kuja kwenye ushirika huo. Labda wamelipokea

Neno na wametenganishwa. Labda wao, wamesamehewa dhambi zao, na kweli, baada ya kusamehewa dhambi zao, wanaweza kutakaswa kutokana na mambo ya ulimwengu, lakini hawajawahi kuingia katika Utukufu huu wa Shekina, itawabidi kuingia kwa ubatizo wa Roho, unaotubatiza katika Mwili huu mmoja wa Utukufu wa Shekina. Ninaomba ya kwamba utafanya hivyo, Bwana.

[182] Ninashukuru sana kwa ajili ya watu hawa asubuhi ya leo waliotangulia kunena mbele zangu, watu mashuhuri, ambao wameshiriki katika jambo hili kuu, labda kabla sijazaliwa. Ni waheshimiwa jinsi gani, jinsi ninavyofurahi sana kuhesabiwa pamoja nao asubuhi ya leo, Baba! Ninaomba ya kwamba baraka Zako za Milele zitakaa juu ya kila mmoja wetu, na jalia hii mikutano iendelee vizuri sana.

[183] Mbariki Ndugu David duPlessis, mbariki Ndugu Carlson, wote, na Ndugu yetu mpendwa Sullivan, na waimbaji hawa wote, na ndugu wa thamani kila mahali, Bwana.

[184] Na dada zetu, Bwana, wakati mwingine ninawazungumzia hao wanawake kwa ukali sana, Ninaomba ya kwamba, Bwana, kamwe hawatapata wazo baya kunihusu mimi. Nilipomwona mwanamke huyo hivi majuzi asubuhi, kasema, "Ulimwongoza kwa Kristo baada ya tisini," Bwana, na—nawataka tu wawe dada, na—na jalia waelewe hilo.

[185] Naomba wahudumu, labda hivyo, kama yule jukwaani hivi majuzi usiku, ulimwita na kumwambia alikuwa akivuta sigara, moja kwa moja jukwaani, jinsi ulivyozitaja dhambi zake, na hata hivyo ni mhubiri! Mungu, na—nampenda ndugu huyo. Ninawapenda hao ndugu wote, lakini kama sikuwapenda, kungekuwa na kasoro kwangu.

[186] Lakini, Bwana, inaponibidi kulizungumzia, jalia wajue ya kwamba si mimi ninayefanya hivyo, huyo ni Roho Wako ambaye—ambaye—ambaye anataja dhambi ya ulimwengu. Nami ninawezaje kunyamaza na kudumisha huduma yangu, Bwana? Siwezi kufanya hivyo. Pia usiwaache wahisi uovu wowote, bali waende tu kwenye Neno na kumtafuta Mungu. Tujalie.

[187] Jalia kila mtu mgonjwa katika Uwepo wa Kiungu asubuhi ya leo, jalia wanyoshe mikono, sasa hivi, wanyakue konzi ya hisopo kutoka katika maisha yao wenyewe, imani ndogo waliyo nayo, kisha upake Damu ya Yesu Kristo mahali hapo pagonjwa, uangalie ikiyeyuka. Ee Mungu, tujalie.

[188] Tusamehe makosa yetu. Wabariki wainjilisti, wachungaji, waalimu, kila mahali, pia jalia mamilioni ya watu bado, waingie katika ushirika huu chini ya Damu ya Mwanao. Tunaomba hayo, katika Jina Lake. Amina.

[189] Mungu awabariki. Ninasikitika kuwaweka wakati huu wote, lakini sikuangalia chini kuona kwamba ilikuwa imechelewa hivyo. Nilifikiri nilikuwa tu hapa yapata ninii-. . .

60-0611B Ushirika
Manchester Hotel
Middletown, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org